BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU TAARIFA YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2019 - 2020

**Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, Muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kufika hapa katika Mkutano huu wa Nne wa Baraza la Kumi katika hali ya uzima wa afya, amani na utulivu na kuweza kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kuwasilisha maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na **Taarifa ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2019 – 2020** ambayo imeandaliwa chini ya kifungu cha **8** cha **Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, nam. 9 ya mwaka 2009**.

**Mheshimiwa Spika,** sina budi kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kutimiza matakwa ya kisheria kwa kuwasilisha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa naomba kuwatambulisha Wajumbe wa Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Machano Othman Said | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Haji Jecha Salum | Katibu |
| 9. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| 10. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani. |

**Mheshmiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na **Taarifa ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2019 – 2020** mbele ya Baraza lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kabisa, dawa za kulevya zinasababisha madhara makubwa katika jamii yetu ambayo yanaathiri kwa kiasi kikubwa kukua kwa maendeleo na ustawi wa jamii yetu nchini. Katika Hotuba yangu hii nitaeleza baadhi tu ya madhara yanayotokana na dawa za kulevya kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika,** watumiaji wa dawa za kulevya hupelekea kupata maradhi mbali mbali kama vile ugonjwa wa mapafu, akili, moyo, utegemezi wa dawa za kulevya, shinikizo la damu na maambukizi ya *VVU/UKIMWI* na homa ya Ini *B* na *C*.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, matumizi ya dawa za kulevya hupelekea uzalishaji mdogo pamoja na kupungua kwa pato la Taifa na familia kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** madhara mengine yanayowapata watumiaji wa dawa za kulevya yanahusishwa zaidi na mfarakano wa kijamii ambapo hupelekea kutengwa na jamii, mmong'onyoko wa maadili na kuongezeka kwa watoto wanaozurura mitaani pamoja na jamii yenyewe kukosa usalama kutokana na kuwepo kwa vitendo vya magenge ya uporaji, wizi, ubakaji na uharibifu wa mali na miundombinu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kuwa, suala la dawa za kulevya ni suala mtambuka, hivyo, Kamati inaishauri Serikali katika marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, nam. *9* ya mwaka *2009*, suala hili la dawa za kulevya

lihamishiwe katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa lengo la kuwapatia mafunzo ya kudandia meli, upekuzi na uzuiaji wa meli (Training in Vessel Boarding, Search and Seizure "VBSS") watendaji sita wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo *(KMKM)* katika Chuo cha Kikosi cha Ulinzi wa Bahari huko *Mahe* nchini *Sychelles* kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani (UNODC), Kamati inashauri kuchukuliwa kwa tahadhari kubwa wakati wa kuwatafuta watendaji hao ili nafasi hiyo isijekutolewa kwa watendaji wasiokuwa na sifa na kuja kupelekea kutofikiwa kwa lengo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** imebainika kuwa, uingizaji wa dawa za kulevya pia unafanyika katika bandari zisizo rasmi, Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu maalum wa kufanya doria za kutosha katika pande zote za bahari nchini katika kuhakikisha kuwa, udhibiti unapatikana katika bandari zisizo rasmi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, rushwa nayo inasababisha uwepo wa dawa za kulevya nchini kutokana na wafanyabiashara wa dawa za kulevya kuwa ni watu wenye fedha nyingi hali inayowafanya kuwa rahisi kutumia fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba malengo waliyojiwekea katika kufanikisha shughuli zao za dawa za kulevya zinafanikiwa, hivyo, Kamati

inaishauri Serikali kuwa inaongeza kasi ya mapambano dhidi ya rushwa ili kwenda sambamba na mapambano ya suala la dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa, mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa la dawa za kulevya mali zake zote zitaifishwe ili iwe funzo kwa wengine.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar kwa juhudi zake za kutoa mafunzo, hata hivyo, bado inaishauri Tume hiyo kuendelea na juhudi za kutoa mafunzo ya ndani hasa kwa kuanzisha mitaala ya elimu kuanzia kiwango cha maandalizi na kuendelea ili watoto wetu waanze kupata ufahamu wa dawa za kulevya na madhara yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza hatua za baadae za Serikali katika kutimiza malengo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi *2020 – 2025* ya kujenga kituo cha Tiba na Marekebisho ya tabia kwa waathirika wa Dawa za Kulevya Pemba. Hatua hii itaweza kuwasaidia wale wote wanaoathirika na matumizi ya dawa za kulevya kwa upande wa Pemba kama ilivyo kwa kituo kama hicho kiliopo Kidimni, Unguja.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kupotea au kupungua kwa baadhi ya vielelezo *(dawa za kulevya)* ambapo hupelekea kesi nyingi kushindwa mahakamani. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuzitaka taasisi zake zinazoshughulikia kesi hasa za

dawa za kulevya kuhakikisha kuwa zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maadili na uadilifu ili haki iweze kutendeka kwa wale wote wanaohusika pamoja na kuhakikisha kuwa vielelezo vyote vinahifadhiwa kikamilifu kuanzia kukamatwa kwake hadi wakati wa kuteketezwa pale kesi inapomalizika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar kuendelea na juhudi zake za kupambana na uingizaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya nchini kwa watendaji wake kupatiwa mafunzo, ujuzi na mbinu za kisasa ili kuliepushia Taifa letu madhara yanayotokana na dawa za kulevya kwa vile waingizaji, wasambazaji na watumiaji wa dawa za kulevya wanatumia mbinu mpya mara kwa mara katika kuhakikisha kwamba malengo yao yanatimia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii na nawaomba Wajumbe wa Baraza hili kutoa michango yao juu ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba Kuwasilisha.

……………………………

*(Mtumwa Peya Yussuf)*

**Makamu Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**

**Baraza la Wawakilishi Zanzibar**